MTIHANI WA KATIKATI YA MUHULA WA PILI 2026
KISWAHILI LUGHA GREDI YA 10
MUDA: SAA 2

JINA……...NAMBARI YA USAJILI……

TAREHE……...SAHIHI……

MAAGIZO KWA MWANAFUNZI:

1. Karatasi hii ina sehemu tano kuu: A, B, C, D na E.
2. Jibu maswali yote kulingana na maagizo katika kila sehemu.
3. Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha sanifu na kwa mwandiko unaosomeka vyema.

SEHEMU YA A: INSHA (Alama 20)

Jibu swali hili la lazima.

1. Wewe ni Katibu wa Kamati ya Usalama katika mtaa wenu. Andika **Kumbukumbu** za mkutano uliofanyika ili kujadili kuzorota kwa usalama mtaani na mikakati ya kukabiliana na hali hiyo. (Alama 20)

SEHEMU YA B: UFAHAMU (Alama 15)

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yote.

Teknolojiya ya kisasa, hasa mitandao ya kijamii, imejitaandika kama ulimi wa pili wa kizazi cha sasa. Vijana wengi wamebobea katika matumizi ya vifaa vya kidijitali kiasi cha kusahau majukumu yao ya kimsingi kama vile masomo na kazi za nyumbani. Hali hii isipotizamwa kwa darubini ya tahadhari, itasababisha mmomonyoko mkubwa wa maadili na utendakazi katika jamii yetu.

Ingawa mitandao hii ina faida tele kama vile kurahisisha mawasiliano na utafiti, upande wake wa giza hauwezi kupuuzwa. Kuna ongezeko la visa vya uhalifu wa kimtandao, upotoshaji wa habari, na mmomonyoko wa lugha sanifu kwani vijana wamebuni lugha ya mkato isiyozingatia sarufi. Ni jukumu la wazazi, walimu, na serikali kushirikiana ili kuongoza kizazi hiki kuelekea matumizi chanya ya teknolojia.